TANGAZO LA SERIKALI NA. 214 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na (16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 667 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya Mwaka 2025, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 15

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 15(2) kwa kufuta maneno "zitawekwa kwenye akaunti ya Halmashauri" na badala yake kuandika maneno "zitarejeshwa kwa mmiliki".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu A, kwa kuongeza maneno "kwa mwezi" mara baada ya neno "mpya" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 6;
(b) katika Sehemu F, kwa kuongeza maneno "kwa wafanya biashara wakubwa" mara baada ya neno "asili" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 10;
(c) kwa kuongeza Kipengele cha 11 kama ifuatavyo:

| Na | Aina ya Shughuli | Kiwango |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| | | cha Ada (Shilingi) |
| "11. | Kibali cha wauzaji wa dawa za asili kwa wafanya biashara wakubwa | 150,000/= kwa mwaka.". |

(d) kwa kufuta Sehemu J na badala yake kuweka kuweka Sehemu ifuatayo:

"SEHEMU J

ADA YA MCHANGO WA MAENDELEO KWA JAMII KUTOKA KWA MAKAMPUNI YANAYOJISHUGHULISHA NA MADINI, TUMBAKU NA MAKAMPUNI MENGINE YALIYOWEKEZA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

| Na. | Aina ya bidhaa/ kampuni | Gharama za ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Makampuni wa Madini | Kwa Mujibu wa kanuni za CSR |
| 2. | Tumbaku | 10/= kwa kila kilogramu moja |
| 3. | Wachimbaji wadogo wa dhahabu | 100/= kwa kila gramu moja |
| 4. | Makampuni mengine yoyote ambayo yanajishughulisha na biashara ya uwekezaji | Kwa mujibu wa makubaliano na Halmashauri.". |

(e) katika Sehemu K-

(i) kwa kuongeza maneno "bei ya soko" mara baada ya neno "kupandwa" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 1;

(ii) kwa kuongeza maneno "bei ya soko" mara baada ya neno "asili" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 2;

(iii) kwa kuongeza maneno "bei ya soko" mara baada ya alfanumeriki "10cm" iliyopo katika safu ya pili ya kipengele cha 4;

(iv) kwa kuongeza maneno "bei ya soko" mara baada ya alfanumeriki "30CM" iliyopo katika safu ya pili ya kipengele cha 5; na

(v) kwa kuongeza maneno "bei ya soko" mara baada ya neno "misitu" iliyopo katika safu ya pili ya kipengele cha 9;

(f) katika Sehemu V, kwa kufuta neno "saba" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 3 na badala yake kuweka neno "nane".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*